

**HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE, KATIKA SHEREHE
YA UZINDUZI WA MAJENGO MAPYA NA YOLIYOKARABATIWA
KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA TABORA, TAREHE 28.06.2010**

**MHE. Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali
za Mitaa, Bibi. Celina Kombani**

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Bwana Abeid Mwinyimusa

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Bwana Mosi Chan'ga

Mwakilishi wa UNHCR Nchini, Bi. Chansa Kapaya

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya wasichana Tabora, Bibi.

Wanafunzi, Wazazi na marafiki wa Shule ya Sekondari Tabora,

Wawakilishi wa Kitongoji cha Ulyankulu,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Ninayo heshima kubwa kujumuika nanyi leo hii katika uzinduzi wa majengo mapya na mengine yaliyokarabatiwa katika Shule ya Wasichana ya Tabora. Ujenzi ambao umetekelezwa kwa

hisani ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR) na Jumuiya ya Kimataifa na kutekelezwa na Jumuiya ya **“Relief to Development Society – REDESO”**; Katika juhudi za kuunga mkono upokewaji wa waliokuwa wakimbizi wa Burundi 162,000 waliokuwa katika kambi, katika Mikoa ya Tabora na Rukwa na ambao sasa wamepata uraia wa kudumu na Serikali ya Tanzania.

Mwezi Julai mwaka jana, nilitembelea Shule hii wakati wa Ziara yangu ya Mkoa wa Tabora. Kwa kweli wakati ule nilisikitishwa sana na hali duni ya majengo yakiwemo mabweni walimokuwa wanalala Wanafunzi.

Hivyo, nina furaha sana leo kuona sifa na hadhi ya Shule ya Wasichana ya Tabora imerudishwa, hususan ikihusishwa na suala jema sana la kushirikisha jamii ya Watanzania katika kuwapokea raia wapya wa nchini na kuwaingiza katika mfumo wa kijamii na kiuchumi wa Tanzania.

Naungana na Mwakilishi wa UNHCR nchini alivyosema kwamba, ni kupitia juhudi kama hizi na miradi ya huduma za jamii, katika maeneo ambapo waliokuwa wakimbizi wanapata uraia wa Tanzania; Ndipo tutaweza kuwapokea na kuwashirikisha katika mfumo wetu wa kijamii wa maisha kwa mafanikio na kuwawezesha kuanza maisha mapya kama raia wa Tanzania na kuepukana na unyanyapaa wa kuitwa wakimbizi.

Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana,

Ningependa kwa dhati kabisa, kutoa shukrani kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Tanzania kwa Jumuiya ya Kimataifa kwa msaada huu uliowezesha ukarabati na ujenzi wa majengo mapya kwa kupitia UNHCR. Hii inaonyesha dhamira yenu thabiti ya kuunga mkono Mkakati kamambe wa Tanzania wa kutafuta suluhisho la kudumu kwa

wakimbizi wa Burundi walioingia nchini mwaka 1972.
Tunawashukuru sana.

Wiki iliyopita, tarehe 22 Juni, 2010 Serikali ya Tanzania ilizindua Mkakati wa Taifa wa Ushirikishwaji Jamii (***National Strategy for Community Integration***); na kuunda mchakato wa kuwahamasisha na kuingiza wakimbizi katika jamii; na kuitaka Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kuisaidia Tanzania ili iweze kutekeleza mpango huu wenye bajeti takriban Dola za Kimarekani Milioni 144.

Manufaa ya Mkakati huu na miradi iliyo chini yake, mfano Ukarabati wa Shule ya Wasichana ya Tabora, yatawafikia wengi, sio tu wanafunzi waliopo hapa leo, na wananchi waliopata uraia hivi karibuni, bali hadi nje ya Tanzania, nchi ambayo waliopata uraia wao hivi karibuni, sasa wanapaita ni nyumbani kwao. Naamini kwamba, mafanikio ya mradi huu yatazitia moyo nchi

zingine zenye matatizo ya muda mrefu ya wakimbizi kuiga mfano wa Tanzania na kuwapatia wahusika uraia.

Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana,

Ningependa kumaliza kwa kutoa ujumbe kwa Wanafunzi waliopo hapa leo kutoka Ulyankulu Sekondari na Tabora Sekondari, na wengine watakaotusikiliza kupitia Vyombo vya Habari. Fursa mliyopata ni tunu ambayo inahitaji uangalizi wa makini, kwani mkiiacha itapotea na kamwe haitarudi tena. Naamini mnatambua thamani halisi ya uwekezaji uliofanywa katika shule yenu. Thamani yake itapatikana ikiwa mtazingatia masomo yenu kwa makini, nidhamu na kuwa na subira katika kuzikabili changamoto zinazoendana na ujana, kwani huu ndio wakati wenu wa kuwekeza kwa ajili ya faida na kwa maisha yenu ya baadae, familia zenu, ndugu zenu, na Taifa lenu la Tanzania.

Aidha naendelea kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa, sekta za kujitolea, sekta binafsi kuwekeza katika elimu, kwani hakuna Taifa lililoendelea bila kuwa na watu walioelimika. Ikiwa kila mtu atatekeleza jukumu lake tutafanikiwa, naamini kabisa inawezekana kufanya haya ya leo sehemu zingine.

Baada ya kusema hayo, sasa ***Nafurahi kutamka kwamba majengo haya mapya yaliyokarabatiwa Yamezinduliwa Rasmi!***

Asanteni kwa kunisikiliza!